



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU ASASI ZILIZOPATA KIBALI CHA KUTOA
ELIMU YA MPIGA KURA NA UANGALIZI WAKATI WA UBORESHAJI WA
DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA MWAKA 2024/2025**

Dodoma, 25 Juni, 2024

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 22 na 24 Juni, 2024, kwa kuzingatia kifungu cha 10(1) (g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024 ikisomwa pamoja na kanuni ya 46(4) ya kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024 imetoa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa asasi za kiraia 157 na kibali cha uangalizi wa uboreshaji kwa asasi 34 za ndani ya nchi.

Asasi zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura zitajulishwa kwa njia ya barua pepe kupitia Mfumo wa Usajili (*Accreditation Management System*) ili kujaza taarifa za kuwawezesha kukamilisha taratibu zingine ikiwemo kutaja maeneo ambayo watatoa elimu hiyo na orodha ya watu watakaotoa elimu ya mpiga kura katika maeneo hayo.

Majina ya taasisi na asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na uangalizi wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura 2024/2025 yatatangazwa kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz na mitandao ya kijamii.

Tume inatumia nafasi hii, kuzipongeza Taasisi na Asasi za kiraia ambazo zimepata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura na kuwa waangalizi wa uandikishaji kwa mwaka 2024/2025.

KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA!!


Kalima, R. K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI